| |
|---|
| **KISWAHILI** |
| **028** |
| **28 /07 /2022 8:30 AM-11:30 AM** |

NESA NATIONAL EXAMINATION AND SCHOOL INSPECTION AUTHORITY

**MTIHANI WA TAIFA KWA SHULE ZA SEKONDARI, 2021-2022**

# SOMO: KISWAHILI

**MCHEPUO:**

- LITERATURE IN ENGLISH -KISWAHILI-KINYARWANDA **(LKK)**
- LITERATURE IN ENGLISH- KISWAHILI- FRENCH **(LKF)**

**MUDA: Masaa matatu**

**MAELEKEZO**

1) **Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.**
2) **Andika majina yako na nambari yako ya usajili kwenye karatasi ya majibu kama vilivyo kwenye fomu yako ya usajili**
3) **Mtihani huu unaundwa na maswali 24**
4) **Mtihani huu unaundwa na sehemu kuu nne:**
   **Sehemu ya I: Ufahamu**: Jibu maswali yote **(alama 25)**
   **Sehemu ya II : Sarufi** : Jibu maswali yote **(alama 25)**
   **Sehemu ya III : Fasihi:** Jibu maswali yote **(alama 30)**
   **Sehemu ya IV : Utungaji** : Jibu maswali kulingana na maelekezo yanayotolewa hasa kwenye swali la '24.c' la kuchagua mada moja. **(alama 20)**
5) **Mwandiko wako usomeke vizuri**
6) **Tumia kalamu ya bluu au nyeusi**

**SEHEMU YA I: UFAHAMU: (Alama 25)**

**Soma kifungu cha habari kifuatacho, kisha ujibu maswali yanayohusika**

**NYAMBERE**

Hapo zamani za kale palikuwa mwanamke mmoja ambaye alizaa watoto wa kike wawili. Mtoto mmoja alikuwa mrembo sana wa sura lakini mwingine alikuwa mbaya sana na mwenye jicho moja bovu. Msichana huyo mrembo alikuwa mnene na aliitwa Mariya. Yule mbaya wa sura alikuwa mwembamba na aliitwa Nyambere.

Nyambere alikuwa na tabia nzuri sana ingawa alikuwa na sura mbaya. Alikuwa anampenda dada yake Mariya lakini Mariya, msichana mwenye kiburi, maringo sana na sura nzuri ya kupendeza, hakumpenda mdogo wake Nyambere. Kila mahali alipotaka kwenda alikuwa hataki kuandamana na ndugu yake Nyambere. Peke yake, alikwenda kwa majirani; shangazi na wajomba zake; Marafiki zake na kwengineko.

Hakuandamana na nduguye maana alifikiri angemtia aibu kwa ajili ya sura yake mbaya. Licha ya kiburi na majivuno, tabia ya umalaya haikukosekana kwake. Angeishi enzi hizi, angeambukizwa magonjwa mengi ya zinaa kama vile UKIMWI.

Siku moja, mwanamume mmoja mtanashati kutoka nchi ya mbali alikuja kumtaka uchumba Mariya maana alikuwa amesikia sifa za uzuri wake. Mwanamume huyu alikuwa si mwanamume hasa, bali zimwi lililokuwa limejigeuza na kuwa binadamu. Basi mwanamume huyu alipomwuliza Mariya kama angeweza kuolewa naye, alikubali bila kusita. Harusi kubwa ilifanyiwa nyumbani kwa wazazi wa Mariya.

Siku ya Mariya kuchukuliwa na mumewe ilipofika, Nyambere alimwambia mama yake, "Mama! Na mimi nitakwenda na dada yangu Mariya". Dada yake aliposikia hivyo alikasirika sana akasema, "Sitaki kwenda na Nyambere. Yeye ni mbaya sana na atanitia aibu kwa wakwe zangu". Mama yao alimbembeleza sana Mariya akasema, "Mariya! Usimchukie ndugu yako. Kumbuka kuwa mlizaliwa na mama na baba mmoja". Kusikia hivyo, Mariya alikubali kwenda naye lakini shingo upande.

Mariya na mume wake pamoja na Nyambere walianza safari yao kuelekea nchi ya mume wa Mariya. Mume wake alikuwa ameandamana na watu wengi sana kutoka nchi yake. Watu hao hawakuwa binadamu bali vichaka ambavyo vilikuwa vimegeuzwa na zimwi hilo kuwa watu. Walipokuwa njiani, watu hawa walianza kutoweka mmoja mmoja na kugeuka tena kuwa vichaka. Mariya alimwuliza mume wake, "Watu wako wameenda wapi?" Mume akajibu, "Wamerudi kwao msituni maana wanaishi msituni". Basi waliendelea na safari yao mpaka wakafika nyumbani kwa zimwi yaani mumewe Mariya. Nyumba ya zimwi ilikuwa kubwa sana.

Ilipofika usiku, mume huyo alingojea mkewe alale fofofo ili kujigeuza kuwa zimwi. Alimchukua Mariya, akamkatakata vipande vipande na, ilipofika asubuhi, aliviunga vipande hivyo tena na kumtengeneza Mariya. Na yeye mwenyewe

alijigeuza kuwa binadamu tena. Alimpatia Mariya chakula kitamu sana maana alikuwa anataka anenepe ili aweze kumla siku moja. Ilikuwa kama kuwekeza mali yako ili uweze kupata faida katika siku zijazo. Mumewe alizidi kufanya maajabu yake wakati wa usiku. Kumbe Nyambere, msichana mwangalifu kuzidi kifani, alikuwa akiyaona yote siku zote. Siku moja, Nyambere alimwambia dadake, "Dada yangu mpendwa, umeolewa na zimwi". Mariya alikasirika sana akasema, "Acha ujinga wako! Mimi nitakufukuza nyumbani kwangu."

Katika nchi ya mumewe kulikuwako na wanawake wengi ambao walikuwa wameletwa kutoka nchi za mbali na kuolewa huko. Wengi wao walikuwa wamegundua tabia na hali za wanaume wao kuwa hawakuwa watu halisi. Na walipowaona Mariya na Nyambere, waliwasikitikia sana na kuwapenda. Lakini wao hawakujua njia za kujiokoa. Sikitiko kubwa ni kuwa Mariya alipoelezewa habari hii, aliipuuza na kusema kwamba ni uvumi. Mumewe Mariya alikuwa akienda kuwinda msituni kila siku. Msituni, baada ya kujigeuza na kuwa zimwi, alikuwa akifanya kazi ya kung'oa miti mikubwa. Siku moja Nyambere alimchukua Mariya msituni kumwonyesha maajabu ya mumewe. Mariya alipoona mumewe amegeuka kuwa zimwi, alishikwa na woga na kutetemeka ovyo. Ndipo aliyaamini maneno ya ndugu yake. Maajabu mengine aliyoyafanya ni kama Kuning'inia kwenye paa; Kula mijusi kafiri ambayo haikupikwa; kujigeuza kuwa kware na kadhalika.

Wakati huo, alishangazwa na kumwona mumewe akiing'oa miti mikubwa sana na kumwambia ndugu yake, "Nyambere, tutatoroka vipi?" Nyambere alimjibu, "Usiwe na woga nitatafuta njia ya kujiokoa".

Wakati wa madhara makubwa, Mola huwanusuru wanawe. Basi Nyambere, kwa kutumia vijiti na nguvu zake za kichawi za kuvifanya vitu mbalimbali viruke angani, aliitengeneza ndege na kuweka mlango mdogo. Ndege hii iliitwa "Mangera". "Mangera" ilipokuwa tayari wakati wa jioni, Mariya na Nyambere waliingia ndani na kupaa juu kuelekea nchi yao.

Punde si punde, mumewe Mariya alirudi nyumbani na kuita, "Mariya! Mariya eh! Fungua mlango". Yeye hakusikia jibu lolote. Aliita mara ya pili, "Nyambere! Nyambere!" Ndipo aliposikia sauti nyororo, "Niko chumbani!" Alipoingia chumbani hakuona mtu. Kumbe ilikuwa sauti ya kasuku aliyekuwa akiyarudia maneno ya Nyambere kabla ya kutoroka. Ndipo kasuku alimwambia, "Ni mimi kasuku!" Mume wake Mariya alijibu, "Acha we!"

Alipotoka nyumbani na kwenda nje, ndipo aliiona "Mangera" angani na kusikia Mariya na Nyambere wakiimba wimbo huu: "Ndege yangu, kimbia, kimbia! Nipeleke nyumbani, kimbia, kimbia!"

Mume naye alijigeuza kuwa zimwi na kuanza kupaa juu akiwafuata Mariya na nduguye. Nyambere alipoona zimwi linawakaribia, alikunya mavi halafu mlima mrefu sana karibu kugusa mbingu ulitokea. Zimwi lilipoanza kuupanda mlima, Nyambere alikojoa mkojo mkali na ikatokea bahari pana na yenye kina kirefu sana. Zimwi lilipojaribu kuogelea lilizama ndani ya bahari na kuaga dunia.

Mariya na Nyambere waliendelea na safari yao na kufika mahali walikozaliwa. Mariya alimwomba msamaha Nyambere kwa chuki aliyokuwa amemfanyia. Alimshukuru pia kwa kuweza kumwokoa katika hatari iliyokuwa imemkabili. Hapo

ndipo Nyambere alifahamu methali isemayo kuwa "Damu nzito kuliko maji." Waliishi pamoja kwa muda mrefu, wakaolewa na bwana mmoja na kukaa kwa raha mstarehe mpaka mwisho wa maisha yao. Huu ndio mwisho wa hadithi.

**Jibu maswali yafuatayo kuhusu kifungu cha habari kilicho hapa juu**

1) Toa sifa za wasichana wawili wanaotajwa katika kifungu cha habari. **(alama 4)**

2) Mariya alipoolewa hakutaka kwenda nyumbani kwake pamoja na Nyambere. Ni kwa sababu gani? **(alama 2)**

3) Ilikuwaje ili Nyambere akubali kwenda na Mariya nyumbani kwake? **(alama 2)**

4) Mme wake Mariya alikuwa na lengo gani alipomfikisha Maria nyumbani kwake? **(alama 2)**

5) Thibitisha kwamba Nyambere alikuwa msichana mwangalifu. **(alama 3)**

6) Nyambere na Mariya weliwezaje kumtoroka mume wake Mariya? **(alama 3)**

7) Mume wake Mariya alipojua kwamba mke wake amemtoroka alijaribu kumkimbilia kwa ajili ya kumrudisha nyumbani. Ilikuwaje ili mume wake Mariya ashindwe kumkamata Mariya? **(alama 4)**

8) Fupisha kifungu cha habari ulichosoma hapa juu kwa kueleza funzo lililomo. **(alama 5)**

## SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 25)

9) Ni shughuli zipi zilizochangia kueneza Kiswahili katika sehemu mbalimbali za dunia? **(alama 3)**

10) Panga maneno yafuatayo kwa utaratibu unaofaa **(alama 2)**

a) muhimu-sehemu-insha–yoyote-tatu-kuu-ina

b) mkukusanyiko-aya-sentensi-wazo-moja-wa-zinazoendeleza-ni-

11) Geuza sentenzi zifuatazo katika usemi wa taarifa. **(alama 3)**

a) "Nguo za shule zilichanika. Umepaswa kutafuta nyingine mpya." Mwalimu mkuu alimwambia mtoto.

b) "Mimi sikuiba vitabu maktabani." Kamasa aliapa mbele ya wazazi wake.

c) "Kwa nini umechelewa?" Mwalimu alimuuliza mwanafunzi.

12) Unda sentensi mbili kisha uonyeshe kiima na kiarifu katika kila sentensi. **(alama 2)**

13) Andika sentensi zifuatazo katika wingi. **(alama 4)**

a) Koti langu limechafuka.

b) Shirika lako linajulikana sana.

c) Gari lake ni la kifahari.

d) Jumba letu linapendeza.

14) Nini maana ya uambishaji? **(alama 2)**

15) Unda kienzi kwa kila neno kutokana na maneno yafuatayo: **(alama 4)**

a) imara

b) fupi

c) fedheha

d) Tayari

16) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya visanduku: **(Alama 5)**

- Baba yake anaishi kijijini.

**SEHEMU YA III: FASIHI (Alama 30)**

17) Sanaa ni nini? **(alama 3)**

18) Nini maana ya fasihi. **(alama 3)**

19) Jadili umuhimu wa sanaa katika jamii. **(alama 4)**

20) Eleza maana ya methali zifuatazo: **(alama 5)**

a) Leo ni leo asemaye kesho ni mwongo.

b) Chelewa chelewa utamkuta mtoto si wako.

c) Ndege aamkaye asubuhi hula wadudu watamu.

d) Akili ni mali.

e) Haraka haraka haina baraka.

21) Kila mtunzi wa mashairi au nyimbo ana uhuru katika utunzi. Jadili kuhusu uhuru huo ukitoa mifano. **(alama 6)**

22) Fani na maudhui ni mambo yanayokamilishana katika kazi za fasihi. Kwa mifano thabiti jadili kauli hii. **(alama 4)**

23) Uhakiki wa kazi za fasihi si jambo la hivi karibuni. Eleza. **(alama 5)**

**SEHEMU YA IV : UTUNGAJI (alama 20)**

24)

a) Nini maana ya insha? **(alama 2)**

b) Kwa sababu gani ni lazima utangulizi wa insha uwe wa kuvutia? **(alama 3)**

c) Chagua mada moja utunge insha yenye maneno kati ya 200 na 250: **(alama 15)**

- "Ndege aamkaye mapema hula wadudu watamu".
- "Umleavyo mtoto ndivyo akuavyo"
- "Mchango wa vijana katika maendeleo ya nchi"

**MWISHO !**

UKURASA TUPU